**MKATABA WA AJIRA YA MUDA MFUPI YA UJENZI WA CHEMBA 12, UJENZI WA MAGETI-2,KUFYATUA TOFALI 400 NA KUFYATUA NA KUJENGA NGUZO 136 (100-MARKER POSTS NA 36 NGUZO ZA FENSI MRADI WA UBORESHAJI HUDUMA YA MAJI MJI WA KIOMBOI KUPITIA FEDHA ZA UVIKO-19.(LOT 1)**

**MKATABA HUU** unafanyika leo tarehe ....10.... mwezi ....4............, 2022

**BAINA YA**

**MKURUGENZI MTENDAJI MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MANISPAA YA SINGIDA (SUWASA), MKOA WA SINGIDA S.L.P 174** (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "**Mwajiri** au **SUWASA**") kwa upande mmoja;

**NA**

**Ndugu.** ....SULEHMAN OMARI.... (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "**Mwajiriwa** au **Fundi**") kwa upande mwingine.

**KWAMBA** kwa pamoja Mwajiri na Mwajiriwa watajulikana kama "**pande mbili za Mkataba**"

**AMBAPO:**

a) Mwajiri ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya maji Safi na Usafi wa Mazingira Manispaa ya Singida mwenye jukumu la kutekeleza ujenzi wa miradi ya maji ya Mji wa Kiomboi,Manyoni-Itigi na Manispaa ya Singida ya uboreshaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira kupitia Fedha za UVIKO-19 yenye makao makuu yake Manispaa ya Singida;

b) Mwajiriwa ni mtu binafsi anayefanya shughuli zake binafsi za ujenzi, Kilimo na biashara katika Mkoa wa Singida

c) Mwajiri anakusudia kumwajiri Mwajiriwa kwa kipindi cha muda mfupi wa siku thelathini (30);

Mwajiriwa anakubali matakwa ya Mwajiri na anakubali kwa hiari yake mwenyewe kuajiriwa kwa muda mfupi kama Fundi wa ujenzi wa chemba 12, Ujenzi wa Mageti-02,Kufyatua Tofali 400 pamoja na kufyatua na kujenga Nguzo 136 mradi wa Uboreshaji huduma ya maji Mji wa Kiomboi.

CamScanner

**MKATABA HUU UNASHUHUDIA** kwa pande zote mbili kukubaliana kama ifuatavyo:

**1. MADHUMUNI YA MKATABA**

Mkataba huu ni kwa ajili ya **Kujenga Chemba 12,kujenga Mageti 02,Kufyatua Tofali 400 pamoja na kufyatua na kujenga Nguzo 136** ambapo Mwajiriwa atapaswa kufanya kazi zote zilizoorodheshwa na kama zinavyofafanuliwa katika **Hati Msako (Quotation)** iliyoambatishwa na mkataba huu.

**2. MUDA WA UTEKELEZAJI WA KAZI**

Kazi hii itafanyika kwa muda usiozidi **siku thelathini** (30) ambapo itaanza **tarehe** 10/4/**2022** na itakamilika **tarehe** 30/05**/2022**.

**3. MALIPO YA UTEKELEZAJI WA KAZI**

a) Mwajiriwa atalipwa jumla ya kiasi cha **Tshs** 11,646,000/- **(Shilingi** MILIONI KUMI NA MOJA LAKI SITA [illegible] ELFU TU) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi husika;

b) Malipo ya Mwajiriwa yatakuwa ni kwa fedha za kitanzania tu (*Tanzanian Shillings*);

c) Malipo hayo yatalipwa aidha kwa fedha taslimu au hundi ambayo italipwa benki;

d) Malipo ya Mwajiriwa yatalipwa kwa awamu zisizozidi tatu (3) kama ifuatavyo:

   i. Malipo ya awamu ya kwanza yatafanyika mara baada ya kazi yote kukamilika kwa 30% ya mkataba.

   ii. Malipo ya awamu ya pili yatafanyika mara baada ya kazi yote kukamilika kwa 70% ya mkataba.

   iii. Malipo ya awamu ya tatu yatafanyika mara baada ya kazi yote kukamilika kwa 100% ya mkataba.

e) Kabla ya malipo ya mwisho kufanyika, mwajiriwa anapaswa kuwasilisha taarifa zote zinazohitajika na kufanya marejesho ya vifaa vyote vya kazi na fedha za mradi kama zitakuwepo



CamScanner

**4. HAKI NA WAJIBU WA MWAJIRI**

Mwajiri ambaye atawakilishwa na msimamizi wa kazi, atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

a) Kutoa vifaa vyote vya ujenzi (materials) kwa fundi kwa wakati

b) Kusimamia na kuthibitisha ubora wa kazi inayofanywa na fundi.

c) Kuwasiliana na uongozi wa eneo husika namna ya kuwashirikisha wananchi/Jumuiya ya watumia maji katika shughuli za ujenzi wa mradi.

d) Endapo kazi iliyofanywa na mwajiriwa haikufikia viwango vya ubora unaotakiwa, Mwajiri atachukua hatua stahiki juu ya mwajiriwa huyo; na msimamizi wa mradi atamtaarifu mwajiriwa kwamba ameshindwa kutimiza masharti ya makubaliano.

e) Kuhakikisha kuwa endapo mwajiriwa atafanya kazi isiyokidhi viwango au isiyoridhisha, mwajiriwa huyo anarekebisha au kurudiwa upya kazi hiyo kwa gharama zake mwenyewe.

**5. HAKI NA WAJIBU WA MWAJIRIWA**

Mwajiriwa ambaye ni fundi atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

a) Kuhakikisha kuwa anatekeleza ujenzi wa kazi zote kama zilivyooelekezwa kwenye sehemu ya 1 (Madhumuni ya mkataba) kulingana na ramani na vipimo vilivyotolewa na mwajiri;

b) Kuhakikisha kuwa anawajibika kufanya kila jambo ambalo kwa ujumla wake litaleta mafanikio kwenye mradi atakao ujenga;

c) Atatekeleza majukumu yake kwa uaminifu, uadilifu, umakini na weledi mkubwa na endapo atatekeleza kinyume na matakwa haya, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake;

d) Atawajibika kwa msimamizi wa mradi (project manager) kwa utendaji wake wa kila siku na atatekeleza maelekezo anayopewa na kiongozi huyo;

e) Atawajibika kuhudhuria mikutano ya tathmini ya mradi pamoja na watendaji wengine wa timu yake kila itakapopangwa;

f) Atawajibika kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mradi kila zitakapohitajika;

g) Kuhakikisha malipo ya vibarua na mafundi walioajiriwa kwa mikataba midogo yanafanyika kwa wakati;



CamScanner

h) Kufanya usafi eneo la ujenzi wa mradi na kuondoa mabaki yote ya vifaa vya ujenzi na kuviweka katika eneo litakaloelekezwa na msimamizi wa mradi;

i) Kuhakikisha kuwa anawapatia matibabu mafundi wasaidizi/vibarua wake mara wapatapo ajali wakiwa kazini au njiani kuelekea/kutoka kazini.

**6. HAKI NA WAJIBU WA MAMLAKA YA MAJI KIUWASA.**

Mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira Kiomboi itakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

a) Kushiriki katika kazi ndogo ndogo za kujitolea kwa ajili ya kushirikiana na mafundi;

b) Kutekeleza majukumu mengine pale inapohitajika kwa maelekezo ya msimamizi wa mradi;

c) Kulinda vifaa vya ujenzi, mitambo na mradi wenyewe ili usihujumiwe.

**7. UTOAJI WA MIKATABA MIDOGO**

a) Mwajiriwa anaweza kuingia mikataba midogo kadhaa ya utekelezaji wa kazi na vibarua (casual labourers) watakaokuwa chini ya usimamizi wake;

b) Mwajiriwa atawajibika kwa jambo lolote linalohusu wafanyakazi (vibarua) wake alioingianao mikataba;

c) Mwajiri hatahusika kwa jamo lolote la wafanyakazi wa mwajiriwa kwa kuwa siyo mwajiri wao.

d) Mwajiriwa atawajibika kupeleka michango ya wafanyakazi wake (vibarua) kwenye taasisi zinazohusika na masuala ya michango kwa wafanyakazi ikiwa ni pamoja na NSSF n.k. na endapo hatafanya hivyo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake na taasisi husika.

e) Mwajiriwa atawajibika kuhakikisha kuwa wafanyakazi wake (vibarua) wanatumia/wanavaa vitendea kazi stahiki wanapokuwa wanafanya shughuli za ujenzi wa mradi ikiwa ni pamoja na kofia ngumu, buti, gloves, nguo za kazi zing'aazo 'reflector' n.k. ili kuepuka kukiuka sheria, kanuni, miongozo na taratibu zinazohusiana na masuala ya OSHA.



CamScanner

**8. UCHELEWESHAJI WA UTEKELEZAJI WA MRADI**

a) Endapo kazi haitakamilika katika muda uliopangwa, mwajiriwa atalipa faini ya asilimia 0.1 ya malipo ya kazi yote kwa kila siku ya ucheleweshwaji, isipokuwa kukiwa na sababu ya msingi ya ucheleweshwaji wa kazi hizo zilizoidhinishwa kwa maandishi na msimamizi wa mradi.

b) Endapo mwajiriwa ataona anashindwa kuanza utekelezaji wa kazi kwa muda /tarehe iliyotajwa kwenye mkataba kutokana na sababu za msingi, atawajibika kutoa taarifa kwa maandishi kwa msimamizi wa mradi akielezea sababu hizo za msingi zinazosababisha ashindwe kuanza utekelezaji.

c) Mwajiriwa anapaswa kuhakikisha kuwa sababu za msingi alizozitoa za kuchelewa kuanza utekelezaji wa mradi zinapata kibali/idhini ya maandishi kutoka kwa msimamizi wa mradi.

d) Endapo mwajiriwa atashindwa kuanza kazi kwa muda uliyopangwa/uliotajwa kwenye mkataba pasipo kutoa sababu za msingi za kufanya hivyo kwa maandishi, msimamizi wa mradi atasitisha mkataba huo kwa manufaa ya umma.

**9. DHAMANA YA UHARIBIFU**

a) Mwajiriwa atawajibika kulipa gharama za uharibifu au madhara yoyote yatakayo sababishwa na wafanyakazi wake au vifaa vyake wakati wa tekelezaji wa mradi;

b) Gharama hizo au madhara hayo yatabainishwa na msimamizi wa mradi kwa maandishi;

c) Mwajiri atakata gharama za uharibifu huo kwenye malipo ya mwajiriwa;

d) Endapo mwajiriwa atakuwa ameshalipwa fedha zake zote, atawajibika kuwasilisha malipo ya uharibifu uliofanyika na endapo hatafanya hivyo ndani ya muda utakaokuwa umebainishwa kwa maandishi, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

## 10. SHERIA NA LUGHA YA MKATABA

a) Mkataba huu utaongozwa na kusimamiwa na sheria za Tanzania

b) Lugha ya mkataba huu itakuwa ni kiswahili.

## 11. USULUHISHI WA MGOGORO

Endapo kutatokea mgogoro wa aina yoyote baina ya mwajiri na mwajiriwa kuhusu utekelezaji wa mradi huu:

a) Pande zote mbili zitatatua mgogoro huu kwa njia ya amani na mazungumzo ambapo makubaliano ya pande hizi mbili yatapelekea mkataba huu kufanyiwa marekebisho; na

b) Endapo mgogoro huu utashindikana kutatuliwa kwa njia ya amani na mazungumzo, pande zote mbili zinaweza kuchukua hatua stahiki za kisheria kwa mujibu wa sheria za Tanzani.

## 12. KUSITISHA MKATABA

Mkataba huu unaweza kusitishwa endapo upande mmoja au pande zote mbili za mkataba zitashindwa kutekeleza wajibu wake au masharti ya mkataba huu.

## 13. MAREKEBISHO YA MKATABA

Mwajiri na mwajiriwa wanaweza kubadilisha baadhi ya masharti ya mkataba huu kwa makubaliano ya pamoja kwa njia ya maandishi.

## 14. MASHARTI YA NYONGEZA

Masharti mahsusi ya nyongeza kuhusiana na utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na:

a) ..........................................................................................................

b) ..........................................................................................................

c) ..........................................................................................................

CamScanner

**KWA USHUHUDA HUU**, pande zote mbili zinaweka sahihi zao katika mkataba huu siku na tarehe kama ilivyooneshwa hapa chini:

| | |
|---|---|
| **Mkurugenzi Mtendaji**<br>**Mamlaka ya maji Safi na Usafi wa Mazingira Manispaa ya Singida (SUWASA)** | **Mkurugenzi Mtendaji**<br>**Mamlaka ya maji Safi na Usafi wa Mazingira Kiomboi (KIUWASA)** |
| Jina la Mwajiri: HOSEA J.P. MAGHIMBI | Jina la Shahidi: VICTOR G. MTATA |
| Sahihi: (signature) | Sahihi: (signature) |
| Tarehe: 10.04.2022 | Tarehe: 11/04/2022 |
| MANAGING DIRECTOR<br>SINGIDA URBAN WATER & SEWARAGE AUTHORITY | MKURUGENZI MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA (KIUWASA)<br>11 APR 2022<br>KIOMBOI SINGIDA |
| **Local Fundi/Mwajiriwa** | **Shahidi wa Local Fundi/Mwajiriwa** |
| Jina: SULEHMANI OMARI | Jina: ALLY MUSSA |
| Sahihi: (signature) | Sahihi: (signature) |
| Tarehe: 10-04-2022 | Tarehe: 10-04-2022 |